Nina Imani Ya Aina Gani?

na

Ellis P. Forsman

Nina Imani Ya Aina Gani?

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Nina Imani Ya Aina Gani?

Ebr. 11:1-10

Ebr. 11:1-3, "*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudia. Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.*"

Imani ni ujasiri wa uhakika kwa kile tunachokitarajia.

Ni bayana ya mambo yasiyioonekana.

Imani ni **jicho** la nafsi.

Utii ni **mkono** wa nafsi.

Ebr. 11:2, "*Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudia.*" – Mfano kwa wazee wa zamani.

Kwa maana imani yao, wazee wa zamani walipata uthibitisho kutoka kwa Mungu.

- Wakati ujao – mtazamo wa taraja.
- Visivyoonekana – udhihirisho wa ukweli wao.

Imani inayoabudu

- Ebr. 11:4, "*Kwa imani Abili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hiyo ijapokuwa amekufa, angali akinena.*"
- Mwanzo 4:1-5, "*Adamu akamjua Hawa mkewe naye akapata mamba, akamzaa Kaini akasema, nimepata mtoto mwanamume kwa BWANA. Akaongeza akamzaa ndugu yake, Habili. Habili alikuwa mchunga kondoo, na Kaini alikuwa mkulima ardhi. Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi sadaka kwa BWANA. Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. BWANA akamtakabali Habili na sadaka yake; bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana.*"

Abili anatoa dhabihu.

Imani ilimsukuma kuabudu sawasawa na neno la Mungu.

Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Imani huja kwa kulisikia neno la Mungu.

Hivyo tunahitimisha kwamba Mungu alimwambia jinsi ya kuabudu.

Ebr. 11:4, "*Kwa imani Abili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hiyo alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake na kwa hiyo ijapokuwa amekufa, angali akinena.***"**

Ibada yake ya uaminifu (dhabihu) ilionyesha haki yake (ya kuwa sahihi na Mungu).

Aina tatu za dhabihu zinazo tarajiwa kwa Wakristo.

Dhabihu ya sifa, matunda ya midomo yetu (kuomba na kuimba).

Ebr. 13:15, "*Basi kwa njia yake yeye na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani tunda la midomo iliungamayo jina lake.*"

Dhabihu iliyo hai, miili yetu.

Rum. 12:1-2, "*Basi ndugu zangu nawasii kwa huruma zake Mungu itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema ya kumpendeza, na ukamilifu.*"

Zawadi zetu au matoleo kwa Mungu vinatajwa kama dhabihu.

Fil. 4:18, "*Lakini ninavyo vitu vyote na kuzidi, tena nimejaa tele; nimepokea kwa mkono wa Epafrodito vitu vile vilivyotoka kwenu, harufu ya manukato, sadaka yenye kibali, impendezayo Mungu.*"

Uwezo unaendelea – Bado inatuambia.

Mwanzo 4:10, "*Akasema, umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inalilia kutoka katika ardhi."*

Damu yake inalilia nini?

Kwamba ibada tu ya uaminifu ndiyo impendezayo Mungu.

Ebr. 12:24, "*Na Yesu mjumbe wa Agano Jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili.*"

Alifanya dhabihu sahihi – mwanadamu anahitajika kujitoa dhabihu leo.

Rum. 12:1, "*Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana.*"

Imani ya Abili ilikuwa ni imani iliyoonyesha ibada kulingana na neno la Mungu.

Imani itembeayo

- Ebr. 11:5, "*Kwa imani Henoko aliamishwa asije akaona mauti, wala hakuonekana kwa sababu Mungu alimhamisha, maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu.*"
- Mwanzo 5: 22-24, "*Henoko akaenda pamoja na Mungu baada ya kumzaa Methusela miaka mia tatu, akazaa wana waume na wake. Siku zote za Henoko ni miaka mia tatu na sitini na mitano. Henoko akenda pamoja na Mungu, naye akatoweka, maana Mungu alimtwaa.*"

Henoko alitembea na Mungu siku ambayo wengine walikuwa wanakwenda mbali na Mungu.

Mwanzo 6:5, "*BWANA akaona ya kuwa maovu ya wanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni bayana tu siku zote.*"

"Kutembea" uhusiana na jinsi ambavyo mtu anaishi.

Imani za mamna hii inakuwa jinsi Mungu anavyokutaka uishi.

Imani hizi zina uwezo wa kuunda tabia, na haiogopi kifo.

Ufu. 1:18, "*Mimi ni wa kwanza na wa misho, na aliye hai nami nalikuwa nimekufa na tazama ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti na za kuzimu.*"

Yesu anafunguo za mauti na za kuzimu (kaburi).

"Tmetafsiriwa" ndani ya ufalme.

Kol. 1:13, "*Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuamisha na kutuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake.*"

Alimpendeza Mungu.

Maisha yake yalikuwa yanampendeza Mungu. Pasipo imani hatuwezi kumpendeza yeye.

Vipi kuhusu maisha yako? Unaishi namna gani? Kwa kutembea? Kwa kufanya? Kwa kusema? Kanisa? Familia?

Iamani ya Henoko ilikuwa ni imani iliyoishi jinsi ambavyo Mungu alitaka iwe.

Imani itendayo kazi

Nuhu alikuwa na imani itendayo kazi.

- Ebr. 11:7, "*Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari ya mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu aliunda safina apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo na haki.*"

- Mwanzo 6:13-22, "*Mungu akamwambia Nuhu, mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia. Ujifanyie safina ya mti wa mvinje, fanya na nyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami. Hivi ndivyo utakavyoifanya; mikono mia tatu urefu wa safina, mikono hamsini upana wake, na mikono thelathini kwenda juu kwake. Uifanyie safina mwangaza, ukaumalize juu kiasi cha mkono mmoja; ukautie mlango wa safina katika ubavu wake; ukaifanyie dari tatu, ya chini, ya pili, ya tatu. Na tazama nitaleta gharika ya maji juu ya nchi, niharibu kila kitu chenye mwili na pumzi ya uhai, kisiwepo chini ya mbingu kila kilichopo duniani kitakufa. Lakini nitafanya agano langu kuwa thabiti; nawe utaingia katika safina, wewe, na wanao, na mkeo, na wake za wanao, pamoja nawe. Na katika kila kilicho hai chenye mwili, wawili wa kila namna utawaleta ndani ya safina kuwahifadhi pamoja nawe; wawe mume na mke. Katika vyote virukavyo kwa jinsi yake, wawili wa kila namna watakuja kwako ili uwahifadhi. Ukahitwalie chakula cha kila namna, kinacholika, ukakusanye, nacho kitakuwa chakula chenu na chao. Ndivyo alivyofanya Nuhu, sawasawa na vyote alivyomwamuru Mungu, hivyo ndivyo alivyofanya.*"

Nuhu alifanya nini? Alisikia maonyo ya Mungu.

Nuhu alimchukua Mungu kwa maneno yake. Uthibitisho pekee ambayo Nuhu alikuwa nayo kuhusu gharika ni kile Mungu alichomwambia.

Tena tunaona kwamba imani yake ilipatikana katika neno la Mungu.

Nuhu "Andaa" aliandaa safina kwa ajili ya kuokoa familia yake na gharika.

Imani ya jinsi hii "huandaa" mtu kwa ajili ya sikukuu ya hukumu ya Mungu.

Maandalizi ya Nuhu yalihusisha:

- Kazi kubwa ya chombo kikuu – ilikuwa ni safina kuu!
- Kazi iliyochukua muda mrefu – alifanya kazi takribani siku 120 akijenga safina.

Mwanzo 6:3, "*BWANA akasema Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini.*"

Je unafanya kazi? Unafanya nini? Je unaendelea, ukivumilia kwa uaminifu?

Imani inayompendeza Mungu ni imani inayojiandaa kwa ajili ya siku kuu ya hukumu.

Mkristo alitii maonyo ya Kristo akizingatia kuanguka kwa Yerusalemu, mwaka wa 70 A.D.

Mt. 24:16, "*Ndipo walio katika Uyahudi wakimbilie milimani.*"

Je tunatii maonyo ili tusije tukamezwa na dunia leo?

2 Tim. 2:4, "*Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari.*"

Nuhu "alijiandaa" kwa ajili ya Siku Kuu? Wanadamu wanatakiwa wajiandae sasa!

Nuhu afanya kazi kama Mungu alivyo mwagiza.

Mwanzo 6:22, "*Ndivyo alivyofanya Nuhu, sawasawa na vyote alivyomwamuru Mungu, hivyo ndivyo alivyofanya.*"

Sawasawa na vyote alivyoamuru Mungu, hivyo ndivyo alivyofanya. Mungu alifanya ufunuo, Nuhu akafuata.

Ikianzia na nyumba yake mwenyewe. Wokovu wa nyumba ya mtu binafsi ndiyo ya muhimu kwanza.

Imani ya Nuhu ilikuwa mfano kwa ulimwengu ule. Utii wake ulisimama kama hukumu kwa wale ambao hawange mtii Mungu.

Utii wake wa imani unaonyesha haki yake.

Alifanyika haki kwa kuitii imani.

Nuhu alikuwa mtu wa kwanza katika Biblia kuitwa “mwenye haki” au “adilifu”.

Imani inayotaka

Ibrahimu alikuwa na imani iliyotaka.

- Ebr. 11:8-10, “*Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi, akatoka asijue aendako. Kwa imani alikaa ugenini ka3tika ile nchi ya ahadi, katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile. Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao wenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.*”

- Mwanzo 12:1-3, “*BWANA akamwambia Abramu, toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani, na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.*”

Abramu aliacha nchi yake. Kwa imani alitii na akaitwa “Rafiki wa Mungu”.

Yak. 2:23, “*Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki, naye aliitwa rafiki wa Mungu.*”

Mungu alimwita na akaitika. Abramu alikuwa na imani katika neno la Mungu.

Mwanzo 12:1-3, “*BWANA akamwambia Abramu toka wewe katika nchi yako na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubarii na kulikuza jina lako, nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani, na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.*”

Alifanya uchaguzi sahihi.

Mwanzo 22:1-18, "*Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema mimi hapa. Akasema umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmoja wapo nitakaokuambia. Ibrahimu akaondoka alfajiri, akatandika punda wake, akachukua vijana wawili pamoja naye, na Isaka mwanaye, akachanja kuni kwa ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa akaondoka akaenda mpaka mahali alipoambiwa na Mungu. Siku ya tatu Ibrahimu akainua macho yake akapaona mahali pakali mbali. Ibrahimu akawaambia vijana wake, kaeni ninyi hapa pamoja na punda, na mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu na kuwarudia tena. Basi Ibrahimu akazitwaa kuni na hiyo sadaka, akamtwika Isaka mwanawe; akatwaa moto na kisu mkononi mwake wakaenda wote wawili. Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, Babangu! Naye akasema mimi hapa mwangu. Akasema, Tazama moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa? Ibrahimu akasema Mungu atajipatia mwana kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili pamoja. Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kisha akamfunga Isaka mwanawe, juu ya zile kuni. Ibrahimu akanyosha mkono wake akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe. Ndipo malaika wa BWANA akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema mimi hapa. Akasema usimnyooshee kijana mkono wako, wala usimtende neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee. Ibrahimu akainua macho yake akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova – yire, kama watu wasemavyo hata leo, katika mlima wa BWANA itapatikana. Malaika wa BWANA akamwitw Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni akasema , nimeapa kwa nafsi yangu asema BWANA kwa kuwa umetenda neno hili wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee, katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitazidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao; na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa kuwa umetii sauti yangu.*"

Alikuwa anapenda kumtoa mwanawe. Alitii wakati ambapo dhabihu iliyozingatiwa ilihusika. <u>Utii</u> ni chachu ya jaribio ya Imani!

Alifanya makazi yake ya muda mufupi (aliishi katika madhabahu, siyo "nyumba"

Aliishi katika nchi ya ugenini. Ebr. 11:9, "*Kwa imani alikaa ugenini katika nchi ile ya ahadi katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile.*"

Hebu tufikirie kwamba ulimwengu huu SIYO kwetu. Sisi ni WAPITAJI hapa.

Fil. 3:20, "*Kwa maana sisi wenyeji wetu uko mbinguni kutoka huko tena tunamtazamia mwokozi Bwana Yesu Kristo.*"

Aliutazamia mji wa kimbingu.

Ebr. 11:10, "*Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao wenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.*"

Imani ya Ibrahimu ilitazama zaidi ya ulimwengu huu. Alipenda kuyafanya maisha haya kama safari; na akatamani kuwa na uvumilivu.

Imani kama hii huamini kwamba wakati ujao unaongozwa na uliopo.

Imani inayo mpendeza Mungu ni imani inayotii.

- Yoh. 14:15, "*Mkinipenda, mtazishika amri zangu.*"
- Ebr. 5:8-9, "*Na ingawa ni mwana alijifunza kutii na mates ohayo yaliyompata naye alipokwisha kukamilishwa akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*"

Tunasema, "nataka kusubiri hadi nijue hakika ni wapi ninakwenda"!

Usiseme, "nataka kusubiri hadi niwe na uhakika nitaishi kama Mkristo."

Je unaimani ya aina gani?

Hitimisho

Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"

Mwandishi ametafsiri imani (mistari 1-3), na anatoa mifano ya wanaume wa imani kuu, na kile ambacho imani yao haikumpendeza Mungu.

Pasipo **imani ya jinsi hii** hatuwezi tukampendeza Mungu.

Hii ndio aina ya imani ambayo mwandishi anaandika katika mustari wa 6, ambayo husimama kama hitimisho letu.

Imani yetu ya kumpendeza Mungu lazima iwe:

- Imani **inayoabudu –** inayoabudu sawasawa na agizo la Mungu.
- Imani **inayotembea** – inayobadili tabia na kuishi jinsi Mungu anavyotutaka tuwe.
- Imani **itendayo kazi** – ambayo inaweza kumwandaa mtu binafsi kwa ajili ya siku kuu ya hukumu ya Mungu.
- Imani **inayopenda** – ambayo itatii kila agizo la Mungu – na kutazama zaidi ya ulimwengu huu.

Tunatarajia uaminifu na upatikanaji kutoka katika vitu na kwa watu wengine. Mungu hatarajii mambo kama haya kutoka kwetu? Tatizo ni kwamba katika shughuli zetu za kidini tunajiona sisi wenyewe kama waliojitowa badala ya kufungwa na jukumu. Kwa maana aliyejitowa, karibia kitu chochote inaonekana kukubalika. Kwa maana mtumwa aliyefungwa amabye kazi yake imefungwa, uaminifu unatarajiwa.